

Karibu

Kujiandikisha

Karibu katika maktaba!

Tumefurahi sana kwa vile umetutembelea. Wakati maktaba imefunguliwa unaweza kutumia vitabu na vyombo vingine vyote viliyomo.

Katika maktaba yetu unaweza kuazima vitu vifuatavyo:

- Vitabu
- Majarida
- Vitabu vilivyochapishwa kwa maandishi makubwa
- CD-ROM
- Compact Discs /CD
- Kanda za video
- DVD

Kanuni za kuazima

- Kwa kulipa karo ya mwaka ya € 15€ (7,50€) unaweza kuazima vitabu na vyombo vingine.
- Watoto na vijana chini ya miaka 18 wanaruhusiwa kuazima vitabu bila malipo.
- Kwa kujiandikisha unahitajika kuleta kitambulisho chako na pia kutupatia anwani yako unayotumia sasa.

Ikiwa watoto au vijana wanataka kujiandikisha, tunahitaji sahihi za wazazi au walinzi.

Tafadhalu tumia kwa uangalifu vitabu vyote unavyoazima. Ukipoteza au ukiharibu kitabu, utahitajika kulipa kingine kipyä.

Kurudisha vitabu

Unaweza kutumia vitabu ulivyoazima hadi tarehe ya kuvirudisha.
Vitabu vinaweza kuazimwa kwa muda wa majuma manne.

Rudisha vitabu na vitu vingine vyote ulivyoazima kwa wakati unaofaa, la sivyo utapigwa faini.

Tunefurahi sana kama tungeweza kukukaribisha wewe pia katika maktaba yetu!

stadtbibliothek herne